# AckySHINE.com

# Sheria kuhusu utoaji mimba

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Sheria kuhusu utoaji mimba zinatofautiana kati ya nchi na nchi. Hapa Tanzania utoaji mimba ni kosa la jinai.5 Kosa la jinai linamchukulia mtu hatua aliyetoa mimba na yule aliyemtoa au kumsaidia kutoa mimba. Hata hivyo hapa Tanzania unaruhusiwa kutoa mimba pale tu inapokwepo sababu za kuokoa maisha ya mama mjamzito kama kuna matatizo ya kiafya au pale mimba inatokana na kubakwa.6 Utoaji mimba hufanyika kwa siri. Ni hatari iwapo utoaji mimba utafanyika bila ya utaalamu. Yule anayesaidia kutoa mimba anawajibishwa kisheria. Iwapo utoaji mimba umefanywa na mtu asiye na ujuzi, kwa mama mwenyewe, au kifaa kilichotumika ni kichafu, au majani au dawa zimewekwa ukeni, zinaweza kuhatarisha maisha ya mama. Ni muhimu hata hivyo kujua kuwa wahudumu wengine hutoa huduma baada ya mimba kuharibika kwa wale wanaohitaji msichana au mama, kutokana na matatizo ya utoaji mimba au kuharibika kwa mimba